



**CHUO KIKUU CHA SOKOINE
CHA KILIMO**

MATUKIO YA SUA

Julai - Septemba, 2026



Toleo la 23

Ardhi ni Hazina

YALIYOMO

- 2** SUA yaendelea kuimarisha ufundishaji, utafiti na utoaji wa ushauri wa kitaalamu
- 3** Kafulila: SUA ni nguzo ya maarifa kwa utekelezaji wa FYDP IV
- 4** Mwenyekiti Kamati ya Bunge aipongeza SUA kwa ubunifu, apongeza Serikali kwa uwekezaji
- 5** Biashara ya kaboni yajadiliwa kuboresha masoko endelevu
- 6** Naibu waziri apongeza ushirikiano wa kimkakati katika utafiti na ubunifu
- 7**
 - Prof. Kabudi asisitiza umuhimu wa kuimarisha huduma za afya ya uzazi, elimu na utafiti
 - Dkt. Mwanakhamis Ameir atembelea banda la SUA kwenye maonesho ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu
- 8** SUA yakabidhi samani Kituo cha Polisi kuimarisha huduma za usalama
- 9** Dkt. Masuruli: Ndaki ya Tiba ya Wanyama SUA yachochea mageuzi katika sekta ya mifugo
- 10** SUA, SACIDS yashirikisha wafugaji Merela
- 11** Jokofu la asili kuboresha maisha ya wajasiriamali Mikese, Morogoro
- 12** SUA yaandika historia kwa kuanzisha shamba darasa la kilimo biashara (FFBS)
- 13** Homa ya kiwele yapatiwa ufumbuzi kupitia utafiti wa SUA
- 14** SUA na ICARS wajadili matumizi salama ya samadi kwa afya ya mifugo na binadamu
- 15** Teknolojia mpya ya kilimo yaanza kuwanufaisha wakulima mkoani Manyara
- 16** SUA yasisitiza mawasiliano ya kisayansi kufikisha matokeo ya utafiti kwa jamii
- 17** Mhitimu wa SUA abuni mashine kurahisisha shughuli za kilimo
- 18** Wadau wahimizwa kuweka maslahi ya taifa mbele katika sayansi, tafiti na ubunifu
- 19** Prof. Chibunda aungana na viongozi kutoa pole kizimkazi
- 20** SUA yaipokea rasmi Shule ya Sekondari Mafiga kuimarisha elimu ya amali
- 21** Benedict Mollel "Tikiti" aigeukia teknolojia ya AI, aishukuru SUA
- 22** Wanafunzi SUA waonesha ubunifu wa mavazi katika Maonesho ya Mafunzo kwa Vitendo
- 23** Bonanza la michezo latumika kuwaaga wanafunzi wanaohitimu katika Kampasi ya Mizengo Pinda



BODI YA UHARIRI

WATAALAMU WA MAWASILIANO NA MASOKO

Bi. Suzana Magobeko
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha
Mawasiliano na Masoko

Bw. Asifiwe Mbembela
Afisa Mawasiliano na
Masoko

MHARIRI

Prof. James Nyangas
Mkuu wa Idara ya Elimu ya
Saikolojia na Unasihi

WASANIFU

Bw. Rajab Kimaro
Bi. Jackline Japhet





SUA yaendelea kuimarisha ufundishaji, utafiti na utoaji wa ushauri wa kitaalamu

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimeeleza kuwa kinaendelea kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake makuu ya kutoa mafunzo, kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu pamoja na kuongeza shughuli za uzalishaji mali.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Raphael Chibunda, alisema hayo alipokua anazungumza na waandishi ya habari jijini Dodoma, ambapo amesema SUA inatoa programu mbalimbali zinazohusisha sayansi za kilimo, uzalishaji na tiba ya wanyama wafugwao na wa porini, misitu, uhandisi wa kilimo na uchumi wa kilimo.

Alisema Chuo pia kinatoa mafunzo ya ualimu wa masomo ya sayansi na elimu ya amali, ustawi wa jamii unaohusiana na kilimo, lugha za kigeni pamoja na Shahada ya Mazao ya Nyuki katika Kampasi ya Mizengo Pinda.

Katika eneo la utafiti, Prof. Chibunda alisema SUA imefanya tafiti mbalimbali zinazolenga kutatua changamoto za jamii, ikiwemo utafiti wa panya buku unaolenga matumizi yake katika maeneo muhimu kama utambuzi wa mabomu na utafiti wa TB ambapo kwa sasa Chuo kinafanya kazi na hospitali Zaidi ya 80 nchini.

Alisema tafiti nyingine zimejikita katika kuboresha mbegu ili ziwe na ukinzani dhidi ya magonjwa, uzalishaji wa mbegu mpya, chanjo za magonjwa ya wanyama, mazao ya misitu na ustawi wa jamii.

Prof. Chibunda aliongeza kuwa SUA

imeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na wadau mbalimbali, ikiwemo kushiriki katika uandaaji wa sera, mijadala na maamuzi ya kisera katika maeneo yenye utaalamu wa Chuo.

Alisema chuo kilishiriki kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, hususan katika kuangalia masuala ya mazingira, huku wakulima wakubwa wakitumia utaalamu wa SUA katika masuala mbalimbali, ikiwemo afya ya udongo.

Akizungumzia falsafa ya elimu ya SUA, Prof. Chibunda alisema masomo yayanayotolewa hapa yanasisitiza kujituma na kujitoa na kufanya kazi kwa vitendo, ikiwemo kwenda shambani kulingana na programu anayosoma.

Alisema mfumo huo unalenga kuwajengea wanafunzi uwezo wa kutumia elimu wanayoipata kujiajiri na kukabiliana na mahitaji ya soko la ajira.



Kafulila: SUA ni nguzo ya muhimu katika utekelezaji wa FYDP IV

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimeendelea kuwa na mchango katika maendeleo ya Taifa baada ya kuandaa mhadhara wa wazi ulioangazia nafasi ya Kituo cha Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPPC) katika kufanikisha Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo (FYDP IV).

Akitoa mhadhara huo, Mkurugenzi Mtendaji wa PPPC, Bw. David Kafulila, alieleza kuwa maarifa, teknolojia na ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi ni nguzo muhimu za kuharakisha maendeleo. Alieleza kuwa PPPC huchochea uwekezaji, ubunifu na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Akizungumza kwa niaba ya Makamu Mkuu wa SUA, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Fedha na Utawala), Prof. Amandus Muhairwa, alisema SUA imeendelea kuwa mshirika muhimu wa Serikali katika kuleta maendeleo kupitia uandaaji wa wataalamu wenye ujuzi na umahiri wa kufanya tafiti na ushauri wa kitaalamu katika kuchangia maendeleo ya sekta ya kilimo na Taifa kwa ujumla.

Aliongeza kuwa kuchaguliwa kwa SUA kuwa mwenyeji wa mhadhara huo ni uthibitisho wa nafasi yake kama kitovu cha maarifa na ubunifu katika kuunga mkono utekelezaji wa FYDP IV na mageuzi ya kilimo nchini.

Rasi wa Ndaki ya Kilimo, Dkt. Nyambilila Amuri, alisema mhadhara huo umeongeza uelewa wa wanafunzi na watafiti kuhusu fursa za PPPC, huku ukiimarisha nafasi ya SUA katika kuandaa wataalamu watakasukuma maendeleo ya taifa.



Mwenyekiti Kamati ya Bunge aipongeza SUA kwa ubunifu, apongeza Serikali kwa uwekezaji

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Bi. Husna Juma, amekipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kuendelea kutumia utaalamu, tafiti na ubunifu katika kutatua changamoto za jamii na kuchochea maendeleo ya Taifa.

Bi. Husna ametoa pongezi hizo Agosti 19, 2026, alipotembelea Banda la SUA katika Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika jijini Tanga, ambapo alipata fursa ya kujionea tafiti, bunifu na teknolojia mbalimbali zilizowasilishwa na Chuo hicho.

Mwenyekiti huyo alitoa pongezi za dhati kwa wataalamu na Jumuiya nzima ya SUA kwa kuendelea kuonesha ubunifu, weledi na kujitoa katika kuendeleza elimu, utafiti na uvumbuzi. Alisisitiza umuhimu wa kuendelea kuwekeza katika maarifa na bunifu zenye tija kwa jamii na Taifa.

Aidha, Bi. Husna aliipongeza Serikali kwa kuendelea kuwekeza SUA, akieleza kuwa uwekezaji huo umechangia uboreshaji wa miundombinu, uimarishaji wa shughuli za utafiti na ubunifu, pamoja na ukuzaji wa uwezo wa kitaaluma.



Biashara ya kaboni yajadiliwa kuboresha masoko endelevu

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Chuo Kikuu cha Copenhagen (UC) kupitia Mradi wa Biashara Endelevu ya Kaboni (SUSTCARB) wamefanya warsha yenye lengo la kubadilishana ujuzi na maarifa kuhusu mitaala na masoko endelevu ya biashara ya kaboni.

Akizungumza wakati wa warsha hiyo Mtafiti wa Mradi Prof. Yonika Ngaga kutoka SUA amesema warsha hiyo inalenga kuongeza uelewa wa wadau kutoka taasisi zinazoshiriki katika mradi kuhusu biashara endelevu ya kaboni, kuboresha tafiti katika eneo hilo na kuweka misingi thabiti ya maamuzi katika eneo la biashara ya kaboni.

Nao waratibu wa mrafi huo Dkt. Rose Kicheleri- SUA, Dkt. Mathew Mabele - UDOM na Mtafiti Mkuu Prof. Jens Friis Lund wa Chuo Kikuu cha Copenhagen (UC), kwa pamoja wamesema kuwa mradi huo umekuja wakati muafaka ili kujenga uwezo wa kitaaluma, kuongeza uelewa wa wadau na wanataaluma kuhusu mienendo ya masoko ya kimataifa ya kaboni na jinsi inavyoingiliana na michakato iliyopo inayohusiana na ardhi na matokeo yake kijamii, kiikolojia, kitaasisi na kimaendeleo.

Akifungua warsha hiyo kwa niaba ya Rasi wa Ndaki ya Misitu, Wanyamapori na Utalii, Prof. Ernest Mauya amesema ushiriki wa wadau katika kutoa mawazo kuhusu uboreshaji wa mitaala ni muhimu katika kuongeza uelewa na ushiriki wa jamii katika biashara ya kaboni.

Ameongeza kuwa uwepo wa ufadhili unaotolewa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Denmark (DANIDA) kupitia mradi huo kwa wanafunzi wanaofanya tafiti kuhusu wa wanafunzi wanaofadhiliwa na Mradi huu unaofadhiliwa na DANIDA ili kufanya tafiti katika eneo hili la masoko ya kaboni utasaidia kujenga uwezo



Naibu Waziri apongeza ushirikiano wa kimkakati katika utafiti na ubunifu

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, aliyemwakilisha Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amepongeza ushirikiano wa kimkakati kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Chuo Kikuu cha Aga Khan (AKU), Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST), pamoja na Chuo Kikuu cha Simon Fraser Canada katika kuendeleza utafiti, ubunifu na matumizi ya maarifa kwa maendeleo ya jamii.

Mhe. Wanu alitoa pongezi hizo tarehe 23 Septemba 2026 wakati wa Kongamano la Tatu, lililofanyika katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST), Arusha. Kongamano hilo linawakutanisha wadau kutoka taasisi hizo kwa ajili ya kuimarisha ushirikiano, kubadilishana maarifa na kujadili suluhisho bunifu za changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii. Kongamano lililotangulia lilifanyika mwaka 2025 katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Morogoro.

Akizungumza katika kongamano hilo, Mhe. Wanu alisisitiza umuhimu wa kutumia uchambuzi wa takwimu, sayansi, teknolojia na ubunifu katika kukabiliana na changamoto za kijamii, kuimarisha elimu ya juu na kuchochea maendeleo katika sekta za afya, kilimo na mazingira.

Aidha, Mhe. Wanu alitoa wito kwa watafiti na taasisi za elimu ya juu kuhakikisha matokeo ya tafiti na maarifa yanayozalishwa kupitia ushirikiano huo yanatafsiriwa kuwa suluhisho za vitendo zenye tija na zinazoboresha maisha na ustawi wa Watanzania.

Vilevile, alisisitiza umuhimu wa kuongeza jitihada za utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi na athari zake katika uzalishaji, hususan katika sekta ya kilimo, huku akihimiza matumizi ya matokeo ya tafiti katika kujenga uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuendeleza maendeleo endelevu.



Prof. Kabudi asisitiza umuhimu wa kuimarisha huduma za afya ya uzazi, elimu na utafiti



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Watu Wenye Ulemavu), Prof. Palamagamba Kabudi amesisitiza umuhimu wa kuimarisha huduma za afya ya uzazi, elimu na utafiti katika taasisi za elimu ya juu ili kuwaandaa vijana kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya taifa.

Amesema serikali itaendelea kushirikiana na vyuo vikuu kuhakikisha huduma rafiki za afya zinapatikana kwa vijana ili kupunguza maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI.

Prof. Kabudi ameyasema hayo alipotembelea Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), ambapo amezindua mashine za kisasa za kugawa bidhaa za kinga dhidi ya VVU na UKIMWI pamoja na huduma za upimaji wa VVU kwa siri.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda ametoa shukrani za dhiti kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Afya kwa kuendelea kuunga mkono mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI.

Amesema msaada huo umeimarisha kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa programu za afya, elimu ya kinga na huduma rafiki kwa wanajumuiya wa Chuo.



Dkt. Mwanakhamis Ameir atembelea banda la SUA kwenye maonesho ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu



Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kutoka Zanzibar, Dkt. Mwanakhamis Ameir, ametembelea Banda la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Agosti 18, 2026, katika Maonesho ya Kitaifa ya Wiki ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yanayoendelea mkoani Tanga.

Maonesho hayo yamedhihirisha namna SUA inavyotumia elimu, utafiti na ubunifu katika kuzalisha maarifa na suluhisho zinazolenga kutatua changamoto za jamii na kuchochea maendeleo. Akiwa katika Banda la SUA, Dkt. Ameir amepata fursa ya kuona bunifu, tafiti na bidhaa mbalimbali zinazotokana na ujuzi na utaalamu wa wataalamu na wanafunzi wa Chuo hicho.

Ushiriki wa SUA katika maonesho hayo unaendelea kukitambulisha Chuo kama kitovu cha elimu, utafiti na ubunifu, huku ukitoa fursa kwa jamii kutambua mchango wa SUA katika kuleta suluhisho bunifu kwa maendeleo ya Taifa.



SUA yakabidhi samani Kituo cha Polisi kuimarisha huduma za usalama

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimekabidhi meza tatu na viti vinane kwa Kituo cha Polisi cha SUA, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa huduma za kiusalama ndani ya Chuo na maeneo jirani.

Akikabidhi samani hizo kwa niaba ya Menejimenti ya Chuo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Fedha na Utawala), Prof. Amandus Muhairwa, alisema ushirikiano kati ya SUA na Kituo cha Polisi cha SUA ni muhimu katika kuhakikisha usalama wa watu na mali.

Prof. Muhairwa alisema Chuo kitaendelea kudumisha ushirikiano wa karibu na kituo hicho pamoja na kutoa msaada pale mahitaji yanapojitokeza, kwa kuzingatia uwezo, utaalamu na rasilimali zilizopo SUA.

Alieleza kuwa SUA ina uwezo wa kutengeneza na kukarabati samani kupitia Kiwanda cha Vuyisile Mini Furniture Factory, kilichopo Kampasi ya Solomon Mahlangu, Mazimbu mkoani Morogoro hivyo amekihimiza kituo hicho kuendelea kuwasiliana na Chuo kinapohitaji msaada unaoweza kutolewa kupitia kiwanda hicho.

Kwa upande wake, Mkuu wa Polisi Wilaya ya Morogoro (OCD), SSP Oscar Ngumbulu, aliishukuru SUA kwa msaada huo, akisema umetolewa wakati muafaka kutokana na changamoto ya uhaba wa samani iliyokuwa inakikabili kituo hicho.

SSP Ngumbulu alisema meza na viti vilivyokabidhiwa vitaboresha mazingira ya kazi na kuongeza ufanisi wa askari Polisi katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Aliongeza kuwa Kituo cha Polisi cha SUA kinatoa huduma za kiusalama kwa wanafunzi, wafanyakazi na jamii inayozunguka Chuo, pamoja na wananchi wengine wanaofika kituoni kupata huduma mbalimbali.

Aidha, aliahidi kuwa samani hizo zitatunzwa na kutumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa, huku akisisitiza kuwa Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na uongozi wa SUA katika kuimarisha usalama ndani ya Chuo na maeneo jirani.



Dkt. Masuruli: Ndaki ya Tiba ya Wanyama SUA yachochea mageuzi katika sekta ya mifugo

Daktari wa mifugo mstaafu, Dkt. Bedan Masuruli, amesema Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) imechangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sekta ya mifugo nchini kupitia uzalishaji wa wataalamu wanaotoa huduma kwa wafugaji, kuimarisha uzalishaji wa maziwa na nyama pamoja na kulinda afya ya jamii.

Akizungumza na SUA Media kuhusu miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Ndaki hiyo, Dkt. Masuruli alisema tangu mwaka 1976, Ndaki imepiga hatua kubwa katika kuboresha mafunzo na kuzalisha wataalamu mbalimbali, wakiwemo mawaziri, makatibu wakuu, wakurugenzi na madaktari wa mifugo wanaohudumu katika maeneo tofauti nchini.

Alieleza kuwa ongezeko la uzalishaji wa maziwa, nyama na kuku pamoja na uuzaji wa bidhaa za mifugo nje ya nchi ni miongoni mwa mafanikio yanayotokana na mchango wa wataalamu waliohitimu SUA na kwamba wataalamu hao wameendelea kuwahudumia wafugaji nchini kote kwa kudhibiti magonjwa, kutoa ushauri wa kitaalamu na kusaidia kuongeza tija katika ufugaji.

Aidha, Dkt. Masuruli aliwashauri wanafunzi na wahitimu wa taaluma ya tiba ya wanyama kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kujituma ili kuhakikisha wafugaji wanapata huduma bora na kuendesha shughuli zao kwa faida huku akisisitiza kuwa maendeleo endelevu ya sekta ya mifugo yanahitaji wataalamu wenye ubobevu watakaosaidia kuzuia magonjwa na kuongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo.

Aliongeza kuwa taaluma ya tiba ya wanyama ina mchango mkubwa katika kuhakikisha usalama wa chakula na kuzuia magonjwa yanayoambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu. Kutokana na umuhimu huo, amesisitiza kuendelea kuiimarisha Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya ili izalishe wataalamu zaidi na kutimiza wajibu wake katika kulinda afya ya wanyama, binadamu na maendeleo ya taifa.



SUA, SACIDS yashirikisha wafugaji Merela

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kwa kushirikiana na Kituo cha Umahiri cha Afya Moja (SACIDS), kimesisitiza umuhimu wa kuishirikisha jamii katika tafiti zinazohusu magonjwa ya binadamu na wanyama, hatua inayolenga kuongeza ufanisi wa kubaini, kufuatilia na kudhibiti magonjwa.

Hayo yalielezwa na Prof. Gerald Misinzo, Mhadhiri kutoka Ndaki ya Sayansi ya Afya na Tiba za Wanyama SUA na Mwenyekiti wa Kigoda cha Utafiti cha O. R. Tambo kuhusu Milipuko ya Virusi.

Akizungumza wakati wa ziara ya washiriki wa Warsha ya Mkakati wa Ushirikishwaji wa Utafiti ya Vigoda vya Utafiti vya O. R. Tambo katika Kata ya Merela, Wilaya ya Mvomero, Prof. Misinzo alisema wafugaji na wakulima ni wadau muhimu katika tafiti kwa kuwa wanaweza kutoa taarifa za mapema kuhusu magonjwa na changamoto zinazowakabili.

Alisema pamoja na tafiti nyingi kuchapishwa katika majarida ya kisayansi, ni muhimu kuhakikisha matokeo yake yanawafikia wananchi kwa lugha rahisi na kuwafikia watunga sera ili kusaidia kuboresha mikakati ya kudhibiti milipuko ya magonjwa.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa kutoa elimu kuhusu kinga, ikiwemo chanjo za mifugo.

Kwa upande wao, wafugaji wa Merela walieleza kuwa ushirikiano na watafiti umewasaidia kupata tiba, elimu na ushauri wa kitaalamu kuhusu afya na uzalishaji wa mifugo. Wameiomba Serikali na watafiti kuendelea kuwafikia katika maeneo yao kwa huduma za afya ya mifugo, elimu na tafiti zinazolenga kutatua changamoto zao, zikiwemo upatikanaji wa malisho, dawa na huduma za kitaalamu.

Wawakilishi wa, Jive Media kutoka Afrika Kusini, ambao ni miongoni mwa washiriki wa ziara hiyo, walipongeza ushirikishwaji wa jamii katika tafiti na kusisitiza kuwa watafiti wanapaswa kutumia njia mbalimbali kuwafikishia wananchi matokeo ya tafiti, ikiwemo machapisho, mikutano na picha, kwa lugha rahisi na inayoeleweka.



Jokofu la asili kuboresha maisha ya wajasiriamali Mikese, Morogoro

Wajasiriamali wadogo katika Soko la Lukole, Kata ya Mikese mkoani Morogoro wameanza kunufaika na teknolojia ya jokofu la asili lililobuniwa na kujengwa na watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia Mradi wa UNESCO-TWAS kwa lengo la kuwasaidia kuhifadhi mazao yanayoharibika kwa haraka ikiwemo nyanya, matunda na ndizi.

Wakizungumza wakati wa kupokea jokofu hilo, wajasiriamali hao walisema awali walikuwa wakipata hasara kutokana na mazao kuiva na kuoza ndani ya siku chache endapo hayakuuzwa kwa wakati.

Bi. Zainabu Ally (31), mfanyabiashara ya nyanya, alisema hali hiyo wakati mwingine ilisababisha kupoteza mtaji na kulazimika kusitisha shughuli zake za biashara.

“Tulikuwa tunapata wakati mgumu maana usipouza kwa wakati, nyanya zako zinaanza kuoza na unalazimika kuziua hata kwa hasara,” alisema Zainabu.

Kiongozi wa Mradi huo, Dkt. Nuria Majaliwa alisema teknolojia hiyo ina uwezo wa kuhifadhi nyanya na matunda kwa kipindi cha hadi wiki mbili (siku 14), hivyo kupunguza upotevu wa mazao na hasara kwa wafanyabiashara.

Kwa upande wake, Kiongozi Mwenza wa Mradi, Dkt. Frida Nyamete alisema jokofu hilo litawapa ahueni wajasiriamali kwani hata wanapolazimika kusafiri au kutokuwepo kwenye biashara kwa sababu mbalimbali bidhaa zao zinaweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu bila kuharibika.

Teknolojia hiyo inatarajiwa kuchangia kupunguza upotevu wa mazao, kulinda mitaji na kuongeza kipato cha wajasiriamali.



SUA yaandika historia kwa kuanzisha shamba darasa la kilimo biashara (FFBS)

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimepiga hatua muhimu katika kuimarisha elimu ya kilimo kwa kuanza kufundisha, somo la Shamba Darasa la Kilimo Biashara (Farmer Field and Business School - FFBS) katika programu ya Shahada ya Uzamili ya Ugani, hatua inayolenga kuandaa wataalamu wenye uwezo wa kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo barani Afrika.

FFBS ni mfumo shirikishi unaowawezesha wakulimakujifunza kwa vitendo, kufanya majaribio, kuchambua changamoto zinazowakabili, kubuni suluhisho na kufanya maamuzi kwa pamoja ili kuongeza tija, kipato na usalama wa chakula.

Katika mafunzo hayo, wanafunzi walifanya kazi kwa karibu na vikundi vitatu vya wakulima mkoani Morogoro, wakishiriki shughuli za kilimo kuanzia maandalizi ya shamba hadi mavuno.

Kupitia ushirikiano huo, wakulima walijengewa uwezo katika kilimo biashara, lishe bora, ubunifu, upatikanaji wa masoko, ushirikiano na taasisi mbalimbali ikiwemo TAHA, maafisa ugani, taasisi za mbegu na wadau wengine wa maendeleo ya kilimo.

Wakulima walieleza kuwa ilikuwa ni mara yao ya kwanza kushirikiana kwa karibu na wasomi kwa namna iliyowawezesha pande zote kujifunza kutoka kwa kila mmoja. Walipongeza mbinu hiyo mpya ya kujifunza na kuomba iendelezwe ili kuwafikia wakulima wengi zaidi.

Somo hili limeanzishwa mwaka 2026 kwa ushiriki mkubwa wa Profesa Mshiriki Rasel Madaha wa SUA, ambaye amekuwa miongoni mwa waanzilishi wake. SUA kimekuwa Chuo pekee duniani kufundisha katika mfumo huu wa Shahada ya Uzamili ya Ugani.

Kupitia FFBS, SUA inalenga kuzalisha wataalamu watakaooongoza mageuzi ya ugani na kuwawezesha wakulima wa Afrika kufanya kilimo biashara chenye tija, kuongeza ubunifu, kuunganisha uzalishaji na masoko, kuimarisha lishe bora, kushirikisha jamii katika maamuzi na kuchangia upatikanaji wa chakula cha kutosha na chenye ubora barani Afrika.



Homa ya kiwele yapatiwa ufumbuzi kupitia utafiti wa SUA

Watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia mradi wa NANOCOM, wameendelea kuwafikia wafugaji katika maeneo mbalimbali kwa kuwapatia mafunzo na ushauri wa kitaalamu kuhusu mbinu bora za kudhibiti ugonjwa wa homa ya kiwele (mastitis). Ugonjwa huo huathiri afya ya ng'ombe wa maziwa na kupunguza uzalishaji pamoja na ubora wa maziwa. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea wafugaji uwezo wa kutambua dalili za ugonjwa huo mapema, kuzuia maambukizi na kuboresha usimamizi wa mifugo.

Akizungumza baada ya kutembelewa na watafiti hao, mfugaji Lazaro Rufo kutoka mkoani Arusha alisema mafunzo aliyopata kutoka SUA mwaka uliopita yameleta mabadiliko makubwa katika shughuli zake za ufugaji. Amesema ameanza kutumia mbinu alizofundishwa za kudhibiti homa ya kiwele, jambo lililosaidia kuongeza uzalishaji wa maziwa na hivyo kuinua kipato na uchumi wa familia yake.

Rufo aliipongeza SUA kwa kuendelea kuwafikia wafugaji moja kwa moja mashambani, akieleza kuwa elimu ya kisayansi imekuwa chachu ya kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa. Alisema ushirikiano kati ya watafiti na wafugaji unasaidia kuhakikisha teknolojia na matokeo ya tafiti yanafika kwa walengwa na kutatua changamoto zinazowakabili.

Pamoja na pongezi hizo, aliomba Chuo kuendelea kutoa mafunzo katika maeneo mengine muhimu ikiwemo utengenezaji wa nishati ya kupikia inayotokana na samadi ya mifugo (biogas), pamoja na mbinu bora za kuanzisha na kusimamia mashamba ya malisho ili kuhakikisha mifugo inapata lishe bora mwaka mzima na kuongeza tija katika uzalishaji.

Aidha, alipendekeza kuandaliwa kwa vipeperushi na machapisho ya kielimu yaliyoandikwa kwa lugha rahisi inayoeleweka

Hatua itakayosaidia kuongeza uelewa wa wafugaji wengi zaidi na kuimarisha mapambano dhidi ya homa ya kiwele pamoja na kuboresha sekta ya ufugaji nchini.



SUA na ICARS wajadili matumizi salama ya samadi kwa afya ya mifugo na binadamu

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kupitia Mradi wa ICARS, kimewakutanisha wadau mbalimbali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar katika Jukwaa la Ubunifu (Innovation Platform) kwa lengo la kujadili na kuweka mikakati ya kuimarisha matumizi salama ya samadi, kuboresha afya ya mifugo na kulinda afya ya binadamu dhidi ya magonjwa yanayoambukizwa kati ya wanyama na binadamu.

Jukwaa hilo liliwakutanisha watafiti, wataalamu wa mifugo, maafisa ugani, watunga sera, wawakilishi wa taasisi za Serikali, sekta binafsi na wadau wa maendeleo kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na kujadili suluhisho endelevu kuhusu usimamizi salama wa samadi.

Akifungua jukwaa hilo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu), Prof. Maulid Mwatawala, aliwashukuru wadhamini wa Mradi wa ICARS kwa kuendelea kuiunga mkono SUA katika utekelezaji wa tafiti na ubunifu unaolenga kukabiliana na changamoto za afya ya binadamu, mifugo na mazingira.

Akiwasilisha mada kuhusu mradi huo, Kiongozi wa Mradi wa ICARS, Prof. Robinson Mdegela, alisema mradi umejikita katika kuboresha ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya samadi kwa kuzingatia kanuni za usalama ili kupunguza hatari ya kusambaa kwa vimelea vya magonjwa kupitia kinyesi cha mifugo kinachotumika kama mbolea na wakulima akisema matumizi yasiyo salama ya samadi yanaweza kuchangia kuenea kwa vimelea vinavyosababisha magonjwa na kuongeza usugu wa vimelea dhidi ya dawa.

Kwa upande wake, Dkt. Salum Manyatta, Mkurugenzi Msaidizi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu na mtaalamu wa Afya Moja (One Health), alisema Serikali imeendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kudhibiti magonjwa yanayoambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

Washiriki wa jukwaa hilo waliahidi kuendeleza ushirikiano katika utekelezaji wa mapendekezo yatakayotokana na majadiliano hayo huku wakisisitiza umuhimu wa kuendelea kutoa elimu kwa wafugaji na wakulima kuhusu matumizi salama ya samadi ili kuongeza uzalishaji, kulinda mazingira na kuboresha afya na ustawi wa jamii.





Teknolojia mpya ya kilimo yaanza kuwanufaisha wakulima mkoani Manyara

Wakulima wadogo katika Mkoa wa Manyara wameanza kunufaika na teknolojia mpya ya kilimo iliyobuniwa nchini, inayolenga kuongeza kasi, usahihi na ufanisi upandaji, hivyo kuchangia ongezeko la tija na uzalishaji wa mazao.

Teknolojia hiyo inayojulikana kama “SmartShamba Multi-Crop Planter,” inalenga kutoa mbadala wa kisasa kwa wakulima wanaotegemea zaidi mbinu za jadi katika shughuli za kilimo.

Ubunifu huo umebuniwa na Ibrahim Meshack, mhitimu wa Shahada ya Uhandisi Kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

Kifaa hicho kimeundwa kwa kuzingatia mahitaji halisi ya wakulima wadogo, kikilenga kupunguza muda na nguvu zinazotumika wakati wa upandaji huku ikiboresha mpangilio na usahihi wa uwekaji wa mbegu shambani.

Ubunifu huo unaonyesha namna elimu ya uhandisi inayotolewa SUA inavyoweza kubadilishwa kuwa teknolojia inayotatua changamoto halisi za wakulima.

Ubunifu huo umetambuliwa miongoni mwa

ubunifu bora uliooneshwa katika Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu iliyofanyika Tanga, jambo linaloendelea kuthibitisha mchango wa SUA katika kukuza ubunifu unaolenga maendeleo ya kilimo na ustawi wa jamii.

Mafanikio ya Ibrahim ni kielelezo cha juhudi za SUA katika kuwajengea wanafunzi uwezo wa kubuni, kutatua changamoto na kuanzisha suluhisho zenye thamani kwa Taifa.



SUA yasisitiza mawasiliano ya kisayansi kufikisha matokeo ya utafiti kwa jamii

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kushirikiana na Kituo cha Umahiri cha Afya Moja (SACIDS Foundation for One Health) na wadau wengine wa utafiti, kimeendelea kuimarisha juhudi za kuhakikisha matokeo ya tafiti yanawafikia wananchi na watumiaji wa mwisho. Hayo yalielezwa wakati wa Warsha ya Mkakati wa Ushirikishwaji wa Utafiti ya Vigoda vya Utafiti vya O.R. Tambo, iliyofanyika SUA, 13 Agosti, 2026 ikilenga kuwajengea watafiti uwezo wa kuwasilisha kwa ufanisi tafiti zao ili kuongeza athari zake katika jamii.

Akizungumza katika warsha hiyo, Prof. Gerald Misinzo, Mwenyekiti wa Kigoda cha Utafiti cha O.R. Tambo barani Afrika kuhusu Magonjwa ya Kuambukiza Yanayosababishwa na Virusi, alisema mawasiliano ya kisayansi ni nyenzo muhimu katika kubadilisha matokeo ya utafiti kuwa maarifa yanayoeleweka na kutumika katika jamii. Amesema watafiti wanapaswa kuwasilisha taarifa za kisayansi kwa lugha na njia zinazolingana na mahitaji ya walengwa, ili kuongeza uelewa, ushiriki na matumizi ya matokeo ya tafiti.

Prof. Misinzo alisema tafiti zinazofanywa na Kigoda hicho kwa kushirikiana na SACIDS na wadau wengine zinahusu magonjwa yanayoathiri wanyama na binadamu, yakiwemo homa ya nguruwe ya Afrika, Newcastle na magonjwa ya samaki. Alisema ni muhimu matokeo ya tafiti hizo kuwafikia wafugaji, wataalamu, watunga sera na wananchi kwa wakati, ili kusaidia kuchukua hatua stahiki na kupunguza madhara ya milipuko ya magonjwa.

Aidha, Prof. Misinzo alisisitiza umuhimu wa kutumia teknolojia na majukwaa ya mawasiliano katika kufikisha taarifa za utafiti kwa hadhira pana. Amesema mawasiliano ya kisayansi yanapofanyika kwa ubunifu na kuzingatia mahitaji ya walengwa, yanaweza kuongeza uelewa wa jamii, kuimarisha ushirikiano na kujenga uaminifu katika taarifa za kisayansi.

Kwa upande wake, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo -Taaluma, Prof. Maulid Mwatawala, alisema utafiti haupaswi kuishia katika machapisho ya kitaaluma pekee, bali unapaswa kuwafikia watumiaji wa mwisho. Amesema mafunzo ya mawasiliano ya kisayansi ni muhimu katika kuwajengea watafiti uwezo wa kueleza matokeo ya tafiti kwa lugha rahisi na inayoeleweka kwa jamii.



Mhitimu wa SUA abuni mashine kurahisisha shughuli za kilimo

Mhitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Bw. Joshua Felix, ametengeneza mashine ya kutengeneza matuta (Ridger Machine) yenye uwezo wa kufanya shughuli mbalimbali za kilimo, hatua inayolenga kupunguza matumizi ya nguvu za binadamu na wanyama pamoja na kurahisisha kazi kwa wakulima, hususan wakulima wadogo.

Akizungumza na SUA Media, Bw. Felix, ambaye ni mhitimu wa Shahada ya Uhandisi wa Kilimo kutoka SUA, alisema wazo la kutengeneza mashine hiyo lime-tokana na changamoto zinazowakabili wakulima wanaotumia nguvu kazi kubwa katika kutekeleza shughuli mbalimbali mashambani.

Alisema mashine hiyo imelenga kusaidia kubadilisha mfumo wa kilimo kutoka kwenye utegemezi mkubwa wa nguvu za binadamu na wanyama kwen-da kwenye matumizi ya teknolojia, hatua ambayo inaweza kuongeza ufanisi wa uza-lishaji huku ikipunguza muda na nguvu zinazotumika kufanya kazi shambani.

“Lengo la kutengeneza mashine hii ni kubadilisha mfumo wa kilimo kutoka kwenye matumizi ya nguvu za wanyama na binadamu na kuwasaidia wakulima wa-dogo,” alisema Bw. Felix, akiongeza kuwa mashine hiyo inaweza kutumika kulima, kutengeneza matuta, kupalilia na kufye-ka, hivyo kumwezesha mkulima kufanya shughuli nyingi kwa kutumia mashine moja.

Alieleza kuwa matumizi ya mashi-ne hiyo yanaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa muda unaotumika katika shug-huli za kilimo, ambapo kwa mujibu wake, inaweza kupunguza muda wa kufanya kazi shambani kwa hadi asilimia 90 ikilinga-nishwa na matumizi ya jembe la mkono.



Wadau wahimizwa kuweka maslahi ya taifa mbele katika sayansi, tafiti na ubunifu

Wadau wa sayansi, teknolojia na ubunifu wametakiwa kuweka maslahi mapana ya taifa mbele katika kujadili na kuandaa mikakati ya kuchochea utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Akizungumza katika majadala wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu uliofanyika wakati wa Wiki ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu, Mkurugenzi wa Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Ladislaus Mnyone alisema kufikia malengo ya Dira ya Taifa kunahitaji wadau kuvuka mipaka ya taasisi wanazotoka na kuangalia namna mawazo na utaalamu wao unavyoweza kuongeza ubora wa tafiti na bunifu nchini.

Alisisitiza kuwa wadau wanapaswa kuelekeza nguvu katika kutafuta suluhisho badala ya kulalamikia changamoto, huku wakitoa mapendekezo ya hatua zinazoweza kuchukuliwa na Serikali, sekta binafsi na wadau wengine ili kuimarisha mchango wa sayansi, teknolojia na ubunifu katika maendeleo ya taifa.

Kwa upande wake, Afisa Mikopo wa SUA, Bi. Farida Malya, alisema kuna umuhimu wa kuwa na taasisi mahsusi itakayojikita katika kufanya tafiti zinazolenga kutatua changamoto na kutoa matokeo yenye manufaa kwa taifa.



Prof. Chibunda aungana na viongozi kutoa pole kizimkazi

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Raphael Chibunda, kwa niaba ya Jumuiya ya SUA, aliungana na viongozi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo katika kufika Kizimkazi, Zanzibar, kumfariji Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mhe. Wanu Hafidh Ameir kufuatia msiba wa baba yake mzazi, Mzee Hafidh Ameir.

Septemba 11, 2026, viongozi hao walifika Kizimkazi wakiwa na salamu za pole na faraja kwa Mhe. Wanu Hafidh Ameir na familia yake katika kipindi cha maombolezo kufuatia kuondokewa na mpendwa wao.

Ujio huo ulidhihirisha mshikamano na upendo wa dhati kutoka kwa viongozi na taasisi walizowakilisha.

Katika salamu zao, viongozi hao walieleza masikitiko yao kwa msiba huo na kumfariji Mhe. Wanu Hafidh Ameir pamoja na familia yake, huku wakiwataka kuwa na subira na uvumilivu katika kipindi hicho kigumu cha majonzi.

Kwa pamoja, walitoa salamu za rambirambi na pole za dhati kwa Mhe. Wanu Hafidh Ameir na familia yake wapate nguvu na faraja kutoka kwa Mwenyezi Mungu katika kipindi cha maombolezo na kumuomba Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya marehemu Mzee Hafidh Ameir



SUA yaipokea rasmi Shule ya Sekondari Mafiga kuimarisha elimu ya amali

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimewapokea rasmi watumishi wa Shule ya Sekondari Mafiga kufuatia shule hiyo kuwa chini ya usimamizi wa Chuo, hatua inayolenga kuimarisha utekelezaji wa elimu ya amali na kuboresha mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi.

Akizungumza katika hafla ya kuwakaribisha watumishi hao, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Prof. Raphael Chibunda alisema kuanzia sasa Shule ya Sekondari Mafiga ni sehemu ya SUA, jambo litakaloweza kuimarisha ushirikiano katika utoaji wa elimu bora na kuwaandaa walimu tarajali pamoja na wanafunzi kupitia mazingira ya kujifunzia kwa vitendo.

"SUA ni taasisi ya mafunzo, Sisi sote ni sehemu ya mchakato wa kujifunza na kufundisha. Kila mmoja wetu ana wajibu wa kuiwakilisha vyema taasisi yetu, kwa kuwa SUA ni mfano wa ubora katika elimu na utafiti," alisema Prof. Chibunda.

Aidha, aliwataka watumishi wa shule hiyo kufanya kazi kwa mshikamano na kutumia kikamilifu rasilimali na fursa zinazopatikana chuoni ili kuimarisha ufundishaji, hususan katika masomo ya sayansi, kwa lengo la kuandaa wanafunzi wenye maarifa, ujuzi na uwezo wa ubunifu unaohitajika katika maendeleo ya taifa.

Akizungumza kwa niaba ya walimu, Mkuu wa Shule ya Sekondari Mafiga Bw. Robert Marwa, alisema walimu na wanafunzi wameupokea kwa furaha uamuzi wa shule hiyo kuwa sehemu ya SUA, akisema hatua hiyo itawawezesha wanafunzi kupata mafunzo ya vitendo katika maabara, mashamba darasa na miundombinu mingine ya Chuo.

Kwa upande wake, Kaimu Amidi wa Shule Kuu ya Elimu ya SUA, Dkt. Imelda Gevas, alisema ushirikiano huo unaenda sambamba na mwelekeo wa Serikali wa kuimarisha elimu ya amali kama ambavyo malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inavyoelekeza.





Benedict Mollel "Tikiti" aigeukia teknolojia ya AI, aishukuru SUA

Mhitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Benedict Elphas Mollel, maarufu kwa jina la "Tikiti", ameendelea kujikita katika teknolojia ya Akili Bandia (AI), licha ya kuwa taaluma yake ya msingi ni Kilimo.

Mollel, ambaye alisoma Shahada ya Sayansi katika Kilimo alisema kwa sasa anajihusisha na teknolojia mbalimbali za AI, ikiwemo AI Automation, AI Engineering na AI Visual, pamoja na kushiriki katika miradi mikubwa ya teknolojia.

Akizungumzia shughuli zake za kitaaluma na kitaalamu, Mollel alisema anajishughulisha na utekelezaji wa miradi mbalimbali inayohusisha matumizi ya teknolojia ya akili unde (AI).

Alisema maendeleo yake katika eneo hilo yamejengwa kupitia uzoefu na maarifa aliyoyapata katika safari yake.

Mollel alisema licha ya kusomea Kilimo, elimu ya chuo pamoja na uzoefu alioupata katika maisha vimemsaidia kujenga uwezo wa kujifunza na kufanya shughuli nje ya taaluma yake ya msingi.

Aidha, alitoa shukrani kwa SUA kwa elimu na mazingira aliyoyapata wakati wa masomo, akieleza kuwa chuo hicho kimekuwa sehemu muhimu katika kumjenga na kumpa msingi wa maarifa anaoutumia

hadi sasa katika shughuli zake.

Mollel alisisitiza umuhimu wa kuendelea kujifunza na kutumia fursa zinazopatikana katika teknolojia, akionesha kuwa mtu anaweza kutumia elimu na uzoefu alionao kuingia katika maeneo mapya na kujenga fursa, hata kama hayahusiani moja kwa moja na taaluma aliyosomea.



Wanafunzi SUA waonesha ubunifu wa mavazi katika Maonesho ya Mafunzo kwa Vitendo

Wanafunzi wa Shahada ya Sayansi ya Familia na Mlaji kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wameonesha ubunifu wao katika kubuni na kushona mavazi kupitia maonesho ya mafunzo kwa vitendo ambayo yamelenga kuwaandaa wanafunzi hao kuingia katika soko la ajira na kujiajiri baada ya kuhitimu masomo yao.

Akifungua Maonesho hayo kwa niaba ya Mkuu wa Idara ya Lishe na Stadi za Mlaji yaliyofanyika Julai 17, 2026 chuoni hapo, Dkt. Safiness Msollo alisema maonesho hayo ni sehemu muhimu ya mtaala wa kozi hiyo kwani yanawapa wanafunzi nafasi ya kuonesha maarifa na ujuzi walioupata darasani kwa vitendo na kwamba yanawajengea uwezo wa kujiajiri au kuajiriwa katika sekta mbalimbali mara baada ya kuhitimu.

Naye Mhadhiri kutoka Idara hiyo, Dkt. Zahra Majili, alisema lengo kuu la maonesho hayo ni kuwapa wanafunzi fursa ya kubuni na kutengeneza mavazi yatakayowasilishwa kwa watumiaji ili kupata maoni yatakayoboresha kazi hizo. Alilifafanua kuwa maonesho hayo sehemu ya tathmini ya masomo, ambapo wanafunzi hupata alama kulingana na kiwango cha ubunifu, ubora wa kazi na namna wanavyowasilisha bidhaa zao. Aidha, amewahimiza wanafunzi kutumia maarifa wanayopata chuoni katika maisha yao ya kila siku.

Kwa upande wake, Mwalimu Mary Marcel ambaye hufundisha masomo ya ushonaji wa nguo na ubunifu wa mavazi, alisema wanafunzi wengi wameonesha kiwango kikubwa cha ubunifu katika kushona na kubuni mavazi, pamoja na kuzingatia kanuni za uvaaji, uchanganyaji wa rangi na aina ya mavazi yanayofaa kwa matukio mbalimbali.

Alisema wahitimu wengi wa programu hiyo tayari wamejiajiri, huku wengine wakitumia mitandao ya kijamii kutoa mafunzo kuhusu mitindo na ubunifu wa mavazi. Aidha, aliwahimiza wanafunzi kutumia maarifa na ujuzi wanaoupata kujiajiri na kutengeneza fursa za ajira badala ya kutegemea ajira za kuajiriwa.

Baadhi ya wanafunzi walioshiriki maonesho hayo, akiwemo Beatrice Marya wa mwaka wa tatu na Barton Shoo wa mwaka wa pili wa Shahada ya Sayansi ya Familia na Mlaji, walisema maonesho hayo yamewapa nafasi ya kuingia katika ulimwengu wa kazi na biashara kwa kuwakutanisha na wadau mbalimbali, wakiwemo waajiri na wateja watarajiwa.



Bonanza la michezo latumika kuwaaga wanafunzi wanaohitimu katika Kampasi ya Mizengo Pinda

Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUASO) Kampasi ya Mizengo Pinda, Katavi, imeandaa bonanza la michezo kwa lengo la kuwaaga wanafunzi wa mwaka wa tatu wanaohitimisha masomo yao katika mwaka wa masomo 2025/2026.

Bonanza hilo liliwakutanisha wanafunzi, watumishi na wadau mbalimbali wa Kampasi likiwa na lengo la kuimarisha mshikamano, afya na mahusiano mema miongoni mwa wanajumuiya wa Chuo.

Mgeni rasmi katika bonanza hilo alikuwa Afisa Tawala wa Kampasi, Bw. Holmisdasi Njungani ambaye aliwapongeza wanafunzi kwa ushiriki wao katika michezo mbalimbali, akisema michezo si tu huchangia afya bora, bali pia huimarisha umoja, ushirikiano na kujenga mahusiano miongoni mwa watu wa rika na mazingira tofauti.

Akizungumza na wanafunzi wanaohitimu, Bw. Njungani aliwataka kutumia maarifa na ujuzi walioupata chuoni kwenda kuleta mabadiliko chanya katika jamii na kuwa mabalozi wazuri wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

"Mnapohitimu masomo yenu na kuondoka Chuoni, kuweni mabalozi wazuri wa Chuo katika jamii mtakazoishi na kufanya kazi. Endeleeni kudumisha nidhamu, mshikamano na moyo wa upendo," alisema Bw. Njungani.

Bonanza hilo lilitawaliwa na hali ya furaha, mshikamano na ushindani wa kirafiki kupitia michezo mbalimbali iliyoandaliwa na uongozi wa SUASO, likihitimisha kwa salamu za heri na mafanikio kwa wahitimu wanapojiandaa kuanza hatua mpya ya maisha na taaluma



MATANGAZO

KARIBU UTANGAZE NA SUA FM, 101.1

Kwa Gharama Nafuu

101.1, SUA FM



@sokoineuniversityofagriculture



@SokoineU

Kwa Mawasiliano piga simu



**0655424251
0655370047**

UTALII

KARIBU UTEMBELEE KAMPASI ZA SUA KWA UTALII NA KUJIFUNZA





Jarida limeandaliwa na:
Kitengo cha Mawasiliano na Masoko
S.L.P 3000, Chuo Kikuu, Morogoro, Tanzania
Simu: 255-023-2640006/7/8/9,
Baruapepe: communicationandmarketing@sua.ac.tz